Kuelewa TAA: Muhtasari Mfupi



Idhini ya Awali na Kurejeshewa Gharama

Idhini ya awali inahitajika kwa ajili ya marejesheo yote ya gharama. Ikiwa wafikiri waweza kuhitaji kurejeshewa gharama yoyote inayohitajika, lazima uwasiliane na Trade Adjustment Assistance (Msaada wa Mabadiliko ya Biashara) (TAA) kabla ya kufanya ununuzi wowote.

- ✓ Ili kurejeshewa gharama zilizoidhinishwa awali kutoka TAA, utahitaji kujiandikisha kwa ajili ya kitambulisho cha Mgawaji wa SWIFT. Tafadhali jiandikishe hapa: http://mn.gov/supplier

Vitabu vya kiada, Nyenzo, Sare, na bidhaa za Kompyuta/Teknolojia ya Juu

- ✓ TAA inashughulikia vitabu vya kiada, nyenzo, sare na kompyuta na bidhaa za teknolojia ya juu **zinazohitajika**.
- ✓ Ni lazima uwasiliane na TAA ili kupata idhini ya awali KABLA YA kununua bidhaa zozote ambazo si vitabu vya kiada

Intaneti

- ✓ TAA hukurejeshea gharama ya $25.00 ili kushughulikia gharama zako za intaneti unapochukua angalau darasa moja mtandaoni.

Msaada wa Ziada

- ✓ **Usafiri:** TAA inaweza kukupa msaada wa nauli ya usafiri ulio nje ya eneo la karibu la maili 15 kwenda upande mmoja. Urejeshaji wa gharama za usafiri unaanza baada ya maili ya 15.
- ✓ **Ruzuku ya kujikimu:** Ikiwa una nia ya kudumisha makazi ya pili au unakaa mbali na nyumba yako kwa muda ili kushiriki katika mafunzo ya ana kwa ana, unaweza kustahiki ruzuku ya kujikimu.

Hati Muhimu za Kurejesha

- ✓ **Training Progress Reports (Ripoti za Maendeleo ya Mafunzo) (TPR)**: **zinahitajiwa kila baada ya siku 60** kuanzia mwanzo wa mafunzo ya TAA hadi mwisho wa mafunzo, bila kujali mapumziko wakati wa mafunzo.
- ✓ **Ratiba za Darasa:** wasilisha kwa TAA kabla ya kila muhula mpya
- ✓ **Alama:** zitume kwa TAA baada ya kukamilika kwa kila muhula.
- ✓ **Sifa ya Utambulisho:** wasilisha nakala kwa TAA baada ya kumaliza mafunzo yako

Matarajio

- ✓ **Unapokuwa umesamehewa:** lazima (1) uwasiliane na Mshauri wako wa Dislocated Worker (Mfanyakazi Aliyepoteza Kazi) (DW) kila baada ya siku 30 (2) udumishe kumbukumbu ya utafutaji wa kazi na ajira (3) uonyeshe maendeleo kila baada ya siku 30 kuelekea kujiandikisha katika mafunzo.
- ✓ **Sera ya Ufaulu Mdogo:** ni lazima udumishe alama ya angalau "C" au juu katika madarasa yako yote na usiondoke kwenye masomo wakati TAA inawajibikia gharama.
- ✓ **Ukufunzi:** Ikiwa unapata changamoto kwenye kozi yako, TAA inaweza kumlipa mwalimu.
- ✓ **Mabadiliko:** Katika hali fulani, TAA inaweza kuidhinisha mabadiliko kwenye mpango wako wa mafunzo ulioidhinishwa awali kama vile mabadiliko kwenye aina ya programu yako, kiwango cha shahada, tarehe ya mwisho ya mafunzo au hali ya kuhudhuria muda kamili/muda mfupi. Maombi yote ya mabadiliko yanahitaji wewe au Mshauri wako wa DW kuwasiliana na TAA ili kupata idhini KABLA YA mabadiliko kutekelezwa.

Trade Readjustment Allowance (Posho ya Marekebisho ya Biashara, TRA)

- ▶ Ni lazima uwe umejiandikisha kuhudhuria muda kamili (kama inavyobainishwa na shule) ndipo upokee TRA, hii inajumuisha muhula wa majira ya joto.
- ▶ TRA itaisha siku yako ya mwisho iliyoratibiwa ya mafunzo au kabla ya tarehe hii ikiwa umemaliza wiki zako za TRA zilizopo.
- ▶ Wasiliana na TRA kupitia DEED.TRA@state.mn.us kwa maswali yoyote kuhusu akaunti yako ya UI/TRA